

Nakala za kusaidia:

Nakala za muhimu

- **Maelezo ya Haki (Statement of Rights)**
Haki zako chini ya *Sheria ya Afya ya Akili 2016*

Mwongozo

- **Mwongozo kwa haki za mgonjwa**
- **Agizo la afya la mapema kwa afya ya akili**
mwongozo na fomu ya agizo la afya la mapema
- **Watu waliyechaguliwa wa kusaidika**
mwongozo na fomu ya miadi

Karatasi ya ukweli

- Haki za Mgonjwa
- Jukumu la watu waliochaguliwa wa msaada
- Haki za familia, walezi
na watu wengine wa msaada
- Agizo la afya la mapema na
matibabu ya masharti machache

Vipeperushi

- Watu wanaosaidia
- Haki zako

Kuweza kuona nakala hizi au kwa habari zaidi, tembelea:

www.health.qld.gov.au/mental-health-act

© State of Queensland (Queensland Health) 2017
creativecommons.org/licenses/by/3.0/au

QH841 0117

Sheria ya Afya ya Akili 2016 (Mental Health Act 2016)

Agizo la afya la mapema

(Advance health directives)



Nini maana ya agizo la afya la mapema?

Agizo la afya la mapema ni hati ambayo inakuruhusu kufanya maamuzi kwa ajili yako kuhusu afya yako. Hati hii inaweza kutumika wakati ujao kama wewe hauko vizuri na huwezi kufanya maamuzi.

Chini ya agizo la afya la mapema, unaweza:

- kukubaliana na tiba na huduma ambayo ungependa kupokea
- hali ya tiba na huduma ambayo hutaki kupokea
- kumteua mtu mwingine kufanya maamuzi kuhusu tiba na matunzo yako
- kutoa maoni yako, matakwa na upendeleo kuhusu afya na mambo ya kibinafsi yako.

Unaweza kufanya agizo la afya la mapema wakati wowote unajisikia vizuri na una uwezo wa kufanya maamuzi. Unapaswa kujadili kufanya agizo la afya la mapema na daktari ambaye anaelewa afya yako ya akili.

Je, mamlaka ya matibabu inaweza kufanywa kwa ajili yangu kama nina agizo la afya la mapema?

Mamlaka ya matibabu inatoa mamlaka kwa daktari kutoa tiba na matunzo kwa mtu ambaye ana ugonjwa wa akili, bila ridhaa yao.

Mamlaka ya matibabu haiwezi kufanywa kwa ajiri yako kama una agizo la afya la mapema ambayo inakubaliana na tiba na huduma unayohitaji kupata vizuri tena

Kama agizo la afya la mapema haikubaliani na matibabu na huduma unayohitaji, mamlaka ya matibabu inaweza kufanywa kwa ajiri yako kama vigezo vikali kwa ajili ya kufanya mamlaka ya matibabu ikitumika

Naweza kufanyaje agizo la afya la mapema?

Unaweza kufanya agizo la afya la mapema kwa kusoma na kujaza *Agizo la afya la mapema afya ya akili—mwongozo na fomu (Advance health directive for mental health—guide and form)*, inayopatikana kutoka tovuti ya huduma ya afya ya akili au *Sheria ya Afya ya Akili 2016*.

Kutoa habari zako za afya za sasa

Unapaswa kuuliza agizo la afya yako mapema kuweza kuwekwa kumbukumbu katika rekodi yako ya afya katika huduma ya afya ya akili. Kwa kufanya hivi, daktari watajua umeweka mapema agizo la afya kama wewe ukishindwa kufanya maamuzi kwa ajili yako mwenyewe wakati ujao. Agizo lako litakuwa linapatikana kwa madaktari juu ya huduma ya afya yoyote ya akili katika Queensland.

Wapi naweza kupata msaada kama nahitaji kujua zaidi kuhusu agizo la afya la mapema?

Unaweza kupata habari zaidi kutoka:

- Mshauri wa Haki za Wagonjwa anayejitegemea (Independent Patient Rights Adviser) katika huduma za akili za afya za jamii
- mfanyakazi wa huduma ya afya ya jamii
- tovuti ya *Sheria ya Afya ya Akili ya 2016*.